

# Maana Ya Kuwa RAFIKI

"Usijali, mpendwa wangu…. Nitarudi baada ya muda mfupi……na tutakuwa na muda mrefu mzuri wa kuishi hapo mbele" Maneno haya aliyasema Jake kwa mke wake Nissi… Aliyasema haya muda mfupi kabla ya kupelekwa chumba cha upasuaji… Alikuwa anakwenda kutoa figo yake moja ili amgawie mke wake ambaye figo zake zote mbili zilikuwa hazifanyi kazi.

Niss akatabasamu…huku uso wake ukionyesha huzuni!

"Jipe moyo Nissi… usiogope…bado kungali mchana maadam ninaishi… Ninakupenda sana" Jake alikuwa akijitahidi kuzungumza kwa sauti ya utulivu. Alikuwa akifanya kila liwezekanalo ili kuifanya nafsi na mwili wa mke wake ukae pamoja… Mke wake amekuwa ndiyo maisha yake Jake na pendo lake na kila kitu kwake.

Mambo hayatokei mara zote kama tunavyopenda. Baada tu ya kupewa dawa ya usingizi kwa ajili ya kupasuliwa Jake akapata usingizi wa moja kwa moja… Katika jitihada za Jake kuokoa maisha ya mke wake yeye akapoteza uhai..

Nissi akawekewa figo na akazinduka…zawadi kutoka kwenye moyo wa mme wake…aliudhihirisha upendo wake kwa gharama isiyokifani. Imemgharimu uhai wake! Ni pendo la namna gani hilo…!! (Yoh. 3:16)

Nataka kukuonyesha kitu hapa kimoja kikubwa sana… Hebu safiri nami hadi mahali panapoitwa Kalvari…. Rudisha wakati wako hadi miaka kama 2000 iliyopita uone kuna nini juu ya Kalvari? Iko misalaba mitatu (Yoh. 19:18); miwili kati ya hiyo ni ya wauaji. Sahau habari zake hiyo… Tafakari juu ya msalaba wa katikati, kimeandikwa nini juu yake? "YESU WA NAZARETI MFALME WA WAYAHUDI" (Yoh. 19:19).

Je alikuwa muuaji? La hasha... Yesu ni Mwana wa Mungu. Hajafa msalabani kwa dhambi yake yoyote kwani hakuwa na dhambi. Alikufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote (Yoh. 3:14, 1Yoh. 2:2) yaani kwa ajili yako na mimi!

Huu ni upendo – ni upendo mkuu kupita wote…

Jake alimpenda aliyempenda, mke wake wa moyo na akatoa uhai wake. Lakini, tazama Msalaba wa Yesu! Yeye hajafa kwa ajili ya wale tu wanaompenda, bali hata kwa waliomchukia. Alikufa kwa ajili ya waliomsaliti, waliomdhihaki, waliomtemea mate na kumchoma mkuki, hata kwa ajili ya yule aliyemhukumu kifo (Math. 27:46, Yoh. 19:28-30).

Tazama maumivu makali aliyonayo machoni mwake…. Siyo tu kwa ajili ya mateso ya msalaba bali Yesu alitazama hatima ya wale waliomtesa, akalia! Alipaza sauti akaomba akisema, "Baba uwasamehe maana hawajui walitendalo!" (Luk. 23:34).

Wale waliomchukia walifanya haya bila kuelewa. Maombi yake yalikuwa pia kwa ajili ya Mafarisayo waliomhoji, Viongozi wa Kiyahudi, Kuhani Mkuu

aliyemhukumu, Yuda Iskariyote aliyemsaliti, Mfalme Herode aliyemdhihaki, Pilato aliyemhukumu kifo, Mkuu wa kikosi aliyemsulubisha pamoja na watu wote wakiwemo wewe na mimi tuliompuuza!

Oh! Nawezaje kuinua macho yangu na kumtazama Yesu, akiwa amebeba dhambi zangu wakati nilimhesabu kuwa amelaaniwa na kutengwa na Mungu.. (Gal. 3:13)

Yesu! Ni mimi niliyekusulubisha wewe… Ni mimi niliyekudhihaki, nikisema hukujiokoa mwenyewe kumbe nilikuwa nikiuzuia ukweli kwamba ulikuwapo msalabani kuniokoa mimi!

Nuru iliyowamulika waliokufa ikazimika… Mtakatifu wa Watakatifu akahesabiwa kuwa laana.. Yesu ukafanyika aibu ili kunifanya mimi nisiaibike siku ya mwisho…

Ulidharauliwa na kukataliwa na watu, hata hivyo ungali ukimiliki. Uliishi kwa kunipenda…ukafa kwa kuniokoa….ukazikwa na kuzibeba dhambi zangu zote… ukafufuka toka kaburini, ukanihesabia haki…Nikawa huru Milele! (Math. 28: 1-60, Rum. 5:1-9).

Mtu anayeutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki yake ni upendo mkubwa sana kwa wanadamu. Wewe umenionyesha maana ya upendo mkuu ni nini… Hakika uliutoa uhai kwa ajili yangu wakati nilipokuwa kama adui yako.

Oh! Yesu, nihurumie mimi maskini mwenye dhambi.. Najuta kwa ajili ya yale niliyoyatenda na kwa jinsi nilivyo! Natubu ujinga wangu.. Nisamehe dhambi zangu… Nifanye kuwa mtoto wako! (Yoh. 1:12, 1Yoh. 3:1-2)

Ninajua wewe ni mwingi wa rehema. Najua umenisamehe dhambi zangu… Asante sana Yesu! Jambo moja tu naweza kusema… Ninakupenda Yesu!

Wakati ninaposema nakupenda, ninajua natakiwa kuzishika amri zako….na hii ndiyo amri yako mpendane ninyi kwa ninyi! (1Yoh. 2:3-6)

Rafiki zangu, Yesu, Mungu wa Milele alitupenda wakati tungali wenye dhambi na akachukua umbo la mwanadamu na akaja katika ulimwengu huu na kufa badala yetu ili kulipa gharama ya dhambi zako na mimi! Upokee upendo wake... Yeye ni Mfalme wa Milele! Siku moja MFALME atakuja katika Utukufu, mfalme wa UPENDO. Ishi ukiwa ni rafiki wa Mungu na wa wanadamu pia. Hiyo ndiyo njia pekee ya kufanywa wana na binti za kifalme.

Sasa basi omba maombi haya, ***"Yesu, Nazitubu dhambi zangu…. Ninatambua umeonyesha upendo wako kwangu kwa kufa kwako msalabani! Nihurumie... Nifanye kuwa mtoto wako…… Katika Jina la Yesu. Amen!***

Wako, Katika Jina la Yesu, SHUBHRA SAJU
Tembelea: www.sjmathew.com

Rafiki mpendwa, tupo hapa ili kukusaidia wewe kuandaa maisha yako ya milele pamoja na Yesu. Usisite kuwasiliana nasi:

Tafadhali wasiliana nasi:

Simu:
Pastor Moses Magembe- +255 715 283819/ 784 283818
Capt. Siyame Paul- +255 767 359993
Barua pepe: gospeldsm@gmail.com

**Gospel Campaign Centre,**
**TAG Majumbasita,**
**P. O. Box 77313, Dar es Salaam**
**Tanzania, East Afrika.**